
UNEP katika mwaka wa 2021

# KUSHUGHULIKIA SAYARI



# Kufanya amani na Mazingira



**2021 ulikuwa mwaka ambao masuala ya mazingira yalifikia umaarufu ambao haujawahi kutokea katika ulimwengu. Macho ya ulimwengu yalikuwa kwa Kongamano la Mabadiliko ya Tabianchi la Umoja wa Mataifa (COP26) mjini Glasgow.**

**Ingawa viongozi wetu hawakutimiza ahadi zao kikamilifu, bado kuna fursa ya kuzuia kupanda kwa joto ulimwenguni lisizidi nyuzijoto 1.5. Walioshiriki waliendelea kuufafanua mfumo wa ulimwengu wa bayoanuwai wa baada ya 2020 – ili mataifa yaweze kufikia makubaliano katika COP15 katika mwaka wa 2022. Kasi ya kushughulikia uchafuzi na taka iliongezeka, huku mataifa yakizidi kutazamia mfumo wa kimataifa wa kushughulikia uchafuzi wa plastiki na athari zake zote, pamoja na mifumo na mikataba iliyopo kuhusu kemikali. Maendeleo yalifanywa pia katika COP yakiangazia tambiko la ozoni, zebaki na taka zenye kudhuru.**



Licha ya mafanikio haya, kuna kazi nyingi ya kufanya katika kushughulikia majanga matatu ya sayari mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira na bayoanuwai, na uchafuzi na taka – hasa kadiri fursa ya kujijenga upya kwa njia bora zaidi baada ya COVID-19 inavyoonekana kuwa imepotea. **Global Recovery Observatory** ya Chuo Kikuu cha Oxford, inayoyoungwa mkono na Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), ilionyesha kwamba chini ya asilimia 20 ya jumla ya matumizi ya hela za kuimarisha uchumi yalikuwa ya kutochafua mazingira. UNEP inapofanya maadhimisho yake ya miaka 50, lengo lake la kuhamasisha, kuelimisha na kuwezesha mataifa kuishi kwa kujali mazingira halijawahi kuwa muhimu zaidi.

UNEP katika mwaka wa 2021 iliunga mkono jitihada za ulimwengu za kubadili uhusiano wake na mazingira na kukabiliana na majanga tatu ya sayari kupitia **ripoti ya Kufanya Amani na Mazingira**. Ilifanyia kazi mwongozo unaopatikana kwenye ripoti yake kupitia **Mkakati mpya wa Muda Mfupi** wa 2022-2025 – unaoelenga kujenga mfumo wa UN ulio thabiti zaidi, uliooanishwa zaidi na unaounga mkono hatua ya mazingira ya kuharakisha juhudi za ulimwengu za kutimiza Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu. Na ulisaidia kuongoza hatua tunazohitaji kukabiliana na majanga matatu ya sayari.

UNEP iliandaa sayansi ya tabianchi ili kuongoza watunga sera. Shirika hili lilifanya kazi na sekta za kibinafsi ili kuimarisha ufadhili na msaada kwa kila kitu kuanzia kwa malengo ya kutozalisha gesi chafu hadi kwa masuluhisho yanayotegemea mazingira. UNEP iliunga mkono juhudi za kimataifa za kupunguza uzalishaji wa gesi kali ya ukaa ya methani. Kampeni ndefu iliyoongozwa na UNEP ilipelekea kukomesha kwa matumizi ya madini ya risasi katika petroli, hali itakayookoa maisha ya mamilioni ya watu. UNEP iliunga mkono ushughulikiaji wa sheria ya mazingira katika mwaka ambao Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa lilitambua haki ya kuwa na mazingira safi, mazuri na endelevu.

Uwezo wa UNEP wa kuathiri kwa njia bora ajenda ya mazingira unategemea Nchi Wanachama za UNEP na wabia wanaofadhili na kutetea kazi yake. Katika mwaka wa 2021, michango kwa ufadhili msingi wa UNEP, Hazina ya Mazingira, ilizidi ile iliyopokelewa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. UNEP inathamini sana msaada wote unaotolewa, hasa katika mwaka huu wa pili wa COVID-19.

UNEP itaendelea kujitahidi kuboreka. Nilifurahi kusoma **tathmini** halisi ya UNEP ya Mtandao wa Tathmini ya Utendaji wa Mashirika ya Kimataifa. Ilitia moyo kuona jinsi UNEP ilivyoimarika, lakini pia nilichunguza kwa makini maeneo yanayohitaji kuboreshwa zaidi.

UNEP imetekeleza mengi, lakini ni lazima ijitahidi zaidi. Changamoto iliyo mbeleni ni kubwa. Bado, kuna sababu za kuwa na matumaini. Kama shirika la kisayansi, UNEP inajitahidi kuleta mafanikio, kama ripoti hii ya mwaka inavyoonyesha.

**Inger Andersen**
Anayefanya kazi Chini ya Katibu Mkuu wa UN na Mkurugenzi Mtendaji wa UNEP

# Kufikia Takwimu za UNEP




## DOLA ZA MAREKANI Trilioni 10

**mali** inayosimamiwa na Mpango wa Fedha wa UNEP-unaoendeshwa na washiriki wa **Muungano wa Wamiliki wa Rasilimali Isiyozalisha Gesi Chafu**, waliojitolea kuoanisha uwekezaji wao na hali ya nyuzijoto 1.5.




## 270

**benki** kutoka nchi 66, kufikia mwaka wa 2021, zimejiandikisha katika **Kanuni za Uwajibikaji wa Benki** ili kuoanisha mikakati na mienendo yao na **Malengo ya Maendeleo Endelevu** (SDGs) na **Mkataba wa Paris**.
Pamoja, zinawakilisha asilimia 45 ya rasilimali za benki za duniani.



## 40

**mataifa** yanayosaidiwa kuhamia kwa bidhaa zinazofaana na mazingira kupitia mpango wa UNEP wa **Pamoja kwa Ufanisi**.



## 42,000

**makala ya habari** iliyochapishwa Siku ya Mazingira Duniani na **Muongo wa UN wa Kuboreesha Mifumo ya Ekolojia**.



## Millioni 1.2

**vifo vya mapema** kwa mwaka vilivyozuiwa kupitia **Ushirikiano wa Kimataifa wa Mafuta na Magari yasiyochafua Mazingira** unaoongozwa na UNEP ili kupiga marufuku matumizi ya petroli iliyo na madini ya risasi.



# 70

**kampuni** zinazowakilisha zaidi ya asilimia 30 ya uzalishaji wa mafuta na gesi duniani ziliahidi uwazi zaidi katika kuripoti uzalishaji wa methani kupitia **Ubia wa Mafuta na Gesi ya Methani 2.0.**



# 500

**kampuni kubwa** zilizo na maono yanayofanana ya uchumi unaoondoa taka na kuhimiza matumizi endelevu ya rasilimali ya plastiki isiyokuwa taka kamwe kupitia **Ahadi Mpya za Kimataifa Kuhusiana na Uchumi wa Plastiki** inayoongozwa na UNEP pamoja na Wakfu wa Ellen McArthur.



# 400,000

**vijana** walioshiriki katika programu ya kubadili tabia ya UNEP ya **Wanaharakati wa Kupambana na Plastiki** kuhusu uchafuzi wa plastiki katika nchi 32.



# KUSHUGH
# SAYA

# HULIKIA

# RI

## Hali ya Hewa
## Mazingira
## Kemikali na Uchafuzi

## Kukuza ushughulikiaji mabadiliko ya tabianchi kupitia sayansi

Ripoti ya UNEP ya **Emissions Gap ya mwaka wa 2021: Joto Linazidi** (EGR 2021), iliyotolewa kabla ya COP26, iligundua kwamba **Ahadi Zinazotolewa na Taifa** (NDCs) zitapelekea dunia kuelekea kushuhudia ongezeko la joto ulimwenguni la angalau nyuzijoto 2.7 katika karne hii. Ikiwa ahadi za kutozalisha gesi chafu zingetekelezwa, ongezeko hili lingepungua hadi nyuzijoto 2.2. Ripoti hio ilionyesha pia kwamba washiriki 17 wa G20 wanaokadiria karibu asilimia 70 ya uzalishaji wa gesi chafu majumbani duniani kote wameahidi kwa uthabiti kufikia lengo la kutozalisha gesi chafu. Zaidi ya makala 4,500 katika nchi 104 zilinukuu sayansi na matokeo ya ripoti hiyo - karibu mara mbili zaidi ikilinganishwa na mwaka wa 2020.

Sayansi na data za UNEP zinatolewa kwa watumiaji kutoka nchi 100 kwenye Facebook kupitia **Kituo chake kipya cha Sayansi ya Tabianchi**. UNEP pia ilitengeneza **dashibodi ya hatua** za kushughulikia mabadiliko ya tabianchi ili kusaidia washikadau kupima maendeleo ya kimataifa na kitaifa dhidi ya ahadi za kushughulikia mazingira. Dashibodi hii imetazamwa takriban mara 30,000, na kupendekezwa na Ofisi ya Kitaifa ya Takwimu ya China, Cardiff Metropolitan na Google Classroom.

> **“ Kama ripoti hii ya [EGR 2021] inavyoweka wazi, iwapo nchi zitatimiza NDC zao za 2030 na ahadi za kutozalisha gesi chafu ambazo zilitangazwa kufikia mwishoni mwa Septemba, tutakuwa tukielekea wastani wa ongezeko la joto ulimwenguni linalozidi tu nyuzijoto 2. Uchambuzi wa ziada unapendekeza kwamba ahadi zilizotolewa mjini Paris zingepunguza ongezeko la joto lisizidi nyuzijoto 4."**
>
> **Alok Sharma**, Rais wa COP26.

# Kushughulikia Hali ya Hewa

## Kuchanga fedha ili kukuza uchumi usiozalisha hewa chafu



Majengo yasiyochafua mazingira.
Picha: Shutterstock

## Kujenga majengo na miji endelevu


Pamoja na wabia na **Mfuko wa Mazingira Duniani** (GEF), UNEP ilizindua mradi wa mabilioni ya dola wa **UrbanShift**, unaosaidia zaidi ya miji 20 kutumia mbinu zinazoingiliana kufanya maendeleo mijini na kuunda mustakabali dhabiti usio na gesi ya ukaa. **Muungano wa Kimataifa wa Majengo na Ujenzi** unaosimamiwa na UNEP na kwa ushirikiano na UNEP ulipelekea kuanzishwa kwa Marrakech Global Climate Action na lengo la pamoja la la kupunguza kwa nusu uzalishaji wa gesi katika majengo kufikia mwaka wa 2030 na kutozalisha gesi ya ukaa kabisa kufikia mwaka wa 2050.

## Kuongoza juhudi ulimwenguni ili kupunguza uzalishaji wa methani

UNEP na wabia walizindua **Kituo cha Data ya Methani Duniani**, pamoja na **Muungano wa Mazingira na Hewa Safi** (CCAC) **Tathmini ya Kimataifa ya Methani** ya UNEP, ili kupunguza uzalishaji wa methani, unaosababisha angalau robo ya ongezeko la joto. Tathmini hiyo inaonyesha kwamba uzalishaji wa methani unaosababishwa na binadamu unaweza kupunguzwa kwa hadi asilimia 45 katika muongo huu. Hii itazuia karibu nyuzijoto 0.3 ya ongezeko la joto ulimwenguni kufikia mwaka wa 2045, na kusaidia kuweza kufikia lengo la nyuzijoto 1.5˚C la Mkataba wa Paris huku ikipunguza uchafuzi wa hewa na kutunza mimea.


Dampo la Dandora, Nairobi, Kenya.
Picha: UNEP

Katika **COP26**, zaidi ya nchi 100 zilitia sahihi **Ahadi ya Kimataifa ya Methani** ili kupunguza uzalishaji wa methani katika sekta za mafuta na gesi, kilimo na taka kwa angalau asilimia 30 kufikia 2030 – kupitia ufadhili wa zaidi ya dola milioni 300. Ripoti ya Emissions Gap inaonyesha kwamba lengo hili linaweza kufikiwa kwa gharama ya chini au bila gharama. Zaidi ya kampuni 70 zinazowakilisha zaidi ya asilimia 30 ya uzalishaji wa mafuta na gesi ulimwenguni ziliahidi pia uwazi zaidi katika kuripoti uzalishaji wa methani kupitia **Ubia wa Mafuta na Gesi ya Methani 2.0**. Juhudi za CCAC na Observatory zitatimiza sehemu muhimu katika utekelezaji wa ahadi hizi.





Kuchunguza mradi wa nishati jadidifu.
Picha: Shutterstock

**Mpango wa Fedha wa UNEP** (UNEP FI) unaoongozwa na **Muungano wa Wamiliki wa Rasilimali Zisizozalisha Gesi Chafu** uliongeza karibu maradufu washiriki wake wanaoahidi kuoanisha uwekezaji wao na hali ya nyuzijoto 1.5, kufikia dola za Marekani trilioni 10 katika rasilimali wanazosimamia. Hii inajumuisha baadhi ya wasimamizi wakuu wa bima duniani, wanaotekeleza sera za kukomesha makaa ya mawe na fueli za visukuku. UNEP FI pia ilibuni miungano mingine miwili ya kutozalisha gesi chafu kwa **benki** na **bima**. Kufikia mwaka wa 2021, zaidi ya benki 270 zilijiandikisha kwa **Kanuni za Uwajibikaji wa Benki** ili kuoanisha mikakati na mienendo yao na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Mkataba wa Paris. Pamoja, zinawakilisha asilimia 45 ya rasilimali za benki ulimwenguni na kuhudumia watu bilioni 1.7.

Mfuko unafadhiliwa na wengi wa **Kituo cha Msaada wa Mtaji wa Kuanzisha Biashara**, unaosimamiwa na UNEP, uliongeza uwekezaji kwa miradi inayozalisha kiwango cha chini cha gesi ya ukaa katika nchi 13 zinazositawi – na kupelekea zaidi ya Megawati 1,000 za uzalishaji wa nishati isiyochafua mazingira, makadirio ya kupunguzwa kwa CO2 ya zaidi ya tani milioni tatu kwa mwaka na ajira mpya 10,000.

## Kuimarisha juhudi za kimataifa za kupunguza joto na matumizi bora ya nishati

**Cool Coalition** inayoongozwa na UNEP inasaidia miji ambayo joto linaweza kuongezeka na kufikia kiwango cha nyuzijoto 4 – kama vile Vietnam, ambapo miji mitatu inafanyia majaribio **miongozo** mipya iliyozinduliwa katika COP26. Katika mwaka wa 2021, mradi wa UNEP wa **Pamoja kwa Ufanisi** ulisaidia nchi 40 kuhamia kwa bidhaa zinazofaana na mazingira. Kwa mfano, Brazil, Nigeria na Indonesia zilihamishia masoko yao kikamilifu kwa mwanga wa LED – hivyo kuokoa dola za Marekani milioni 300 kila mwaka za watumiaji bidhaa na kuzuia hitaji la mitambo miwili mikubwa ya kuzalisha umeme.

Wakati huohuo, ripoti ya Jopo la Rasilimali za Kimataifa iliyotolewa na UNEP **Matumizi Mazuri ya Rasilimali na Mabadiliko ya Tabianchi** ilinukuliwa katika mradi mpya wa **Mpango wa Kukuza Uchumi Usiochafua Mazingira** wa Umoja wa Ulaya pia kwa ripoti za mamlaka nchini Uturuki na Afrika Kusini, pamoja na sekta ya kibinafsi inayoongoza ya Deloitte **Mkakati wa Hali ya Hewa Duniani**.



Mradi mpya wa Mifumo wa Kutoa Tahadhari kuhusu Majanga Mapema unaweza kutoa taarifa muhimu ya hali ya hewa nchini Timor-Leste. Picha: Picha ya UN



Kijiji cha Nalma, Nepal. Sehemu kubwa ya ardhi hapa inatumika kukuza mpunga, kukuza bustani na ujenzi. Picha: CIFOR

# Kushughulikia Hali ya Hewa



Mradi wa Mandhari Inayobadilika ya Mawese, Buluq Sen, Kalimantan Mashariki, Indonesia. Picha: CIFOR

## Kukabiliana na athari za tabianchi zinazoongezeka kutegemea eneo

UNEP inazisaidia nchi kuunda Mipango ya Kitaifa ya Kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kutokana na sayansi ya hivi karibuni. **Programu ya Kuwezesha Mikakati ya Kitaifa Duniani Kutegemea Nchi** (NAP-GSP), inayofadhiliwa na GEF na kuendeshwa kwa ushirikiano na UNDP, ilifikia mwisho wake mwaka wa 2021 baada ya kusaidia takribani nchi zinazositawi 60. Wakati huohuo, miradi inayofadhiliwa na UNEP inayotemea eneo ilizinduliwa nchini Djibouti, Lao PDR, Nepal, Sudan Kusini, Uganda na Zambia.

UNEP pia ilizindua hazina mbili mpya za fedha ili **kuimarisha** na **kufadhili** uvumbuzi wa kukabiliana na hali katika nchi zinazoendelea. Mfuko wa Global EbA unatoa mtaji wa kuanzisha biashara kwa ajili ya mbinu bunifu za **kukabiliana na hali kulingana na mfumo wa ekolojia** (EbA), kuanzia kwa utunzaji wa miamba ya matumbawe nchini Ufilipino hadi uboreshaji wa mifumo ya ekolojia ya ukingo wa mito ili kudhibiti mmomonyoko wa udongo nchini Fiji.UNEP pia inafadhili zaidi ya miradi 45 kutegemea eneo ili kuboresha karibu hekta 113,000 za mifumo ya ikolojia kwa manufaa ya watu milioni 2.5 ulimwenguni.

Mradi mpya wa Mifumo wa Kutoa Tahadhari Mapema kuhusu majanga mengi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 21 uliozinduliwa na UNEP nchini Timor-Leste utaimarisha habari kuhusu tabianchi na huduma za maonyo ya mapema kwa idadi yake ya watu milioni 1.3 walio hatarini.

**KUSHUGHULIKIA**
**SAYARI**

## Kujenga jamii thabiti kupitia masuluhisho yanayotegemea mazingira

Kama matokeo ya ushirikiano unaoongozwa na UNEP wa **Blue Forests Solutions** kaboni ya bluu imeaangaziwa katika zaidi ya NDC 30 na kukuza eneo la misitu ya mikoko katika soko la hiari la kaboni mara 25 zaidi.

UNEP pia ilishawishi wafadhili na sekta ya kibinafsi kutoa tani bilioni moja ya upunguzaji wa hewa chafu wa kiwango cha juu kutoka kwa misitu kabla ya mwaka wa 2025 kupitia **Shindano la Green Gigaton**. **Muungano wa LEAF** - unaopelekea matokeo yanayogharimu dola bilioni 1 za Marekani ili kutunza misitu ya tropiki katika nchi zinazoendelea - ulipitisha mfumo huu unaojumuisha sekta za umma na za kibinafsi na kusaidia nchi saba kupata ufadhili wa misitu kwa kiwango kikubwa. Kupitia **UN-REDD**, wito wa muungano wa mapendekezo ya dola milioni 100 za Marekani ulifikiwa na kupita mara kumi zaidi.

Ripoti ya UNEP ya **Hali ya Fedha ya Mazingira** ilitoa wito wa uwekezaji katika masuluhisho yanayotegemea mazingira uongezeke mara tatu kufikia mwaka wa 2030 na kuongezeka mara nne zaidi kufikia mwaka wa 2050. Ilibainisha fursa kwa serikali, mashirika ya biashara na wafadhili kukabiliana na majanga matatu ya sayari. Kama matokeo, taasisi za fedha na biashara za kilimo ziliahidi kutoa **dola za Marekani bilioni 3 kama mikopo na uwekezaji ili kuharakisha utengenezaji wa bidhaa bila nyama na kukuza soya bila kuharibu ardhi** katika eneo la Amerika Kusini.

Mbia wa UNEP **GreenFund** na kampuni ya usindikaji ya vyakula ya Brazili Marfrig walitia sahihi, hazina ya mkopo wa dola milioni 30 za Marekani, **unaohusishwa na uendelevu wa miaka 10** ili kuwezesha kufuga mifugo bila ukataji wa miti katika maeneo ya Amazon na Cerrado, na kufadhili mawese kwa njia endelevu nchini Indonesia na soya nchini Brazili.

## Haki ya kuwa na mazingira safi

Mwezi wa Oktoba mwaka wa 2021, **Baraza la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa** (HRC) lilipitisha azimio kuhusu **haki ya kuwa na mazingira safi, mazuri na endelevu** katika wakati wa mafanikio ya kazi ya haki ya kijamii na kimazingira ya UNEP.

Azimio hilo jipya linatambua uharibifu unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira kwa mamilioni ya watu ulimwenguni pote. Linaangazia kazi ya watetezi wa mazingira katika mfumo wa haki za binadamu na kusaidia kuwalinda wale wanaoteswa kwa kuwa wanaharakati. Linaweza pia kuzipa ujasiri serikali, wabunge, mahakama na makundi ya raia kufuatilia **Ajenda ya Pamoja** ya mshikamano mpya, pamoja na **Wito wa mwaka wa 2020 wa Kushughulikia Haki za Binadamu ya 2020**.




Kundi la wanaharakati wakiandamana kuhusu uharibifu wa mazingira unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Picha: Shutterstock

# Kushughulikia Mazingira



NCAVES nchini Afrika Kusini ilikusanya data kuhusu spishi za mimea ya cycads. Picha: Shutterstock

## Kubadilisha jinsi ya kuwajibikia mtaji wa malighafi

Mwaka wa 2021, **Tume ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa** ilipitisha **Mfumo wa Uwajibikiaji wa Mazingira na Uchumi - Uwajibikiaji wa Mifumo ya Ekolojia** katika kile Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa António Guterres alichoita "hatua ya kihistoria kuelekea kubadilisha jinsi tunavyoona na kuthamini mazingira." Kupitia **mradi** unaotekelezwa na UNEP na UNDESA, Afrika Kusini imekuwa nchi ya kwanza inayoendelea kuzindua **Mkakati wa miaka 10 wa Kuwajibikia Mtaji wa Malighafi**.

UNEP iliwasiliana na zaidi ya nchi na maeneo 200 kukusanya na kuripoti data za viashiria vinavyohusiana na mazingira vya SDG chini ya usimamizi wa UNEP - ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na mwaka wa 2020. Data hii mpya iliyojumuishwa kwa **Hifadhidata ya SDG Ulimwenguni** inasaidia kuziba pengo kwenye data ya viashiria vya SDG.

# Kukuza bayoanuwai ulimwenguni

Katika Oktoba mwaka wa 2021, Washirika wa **Makubaliano ya Uanuai wa Kibayolojia** (CBD) walikusanyika kwa awamu ya kwanza ya **Kongamano la Umoja wa Mataifa la Bayoanuwai**(COP-15) na kujitolea kuendeleza, kupitisha na kutekeleza mfumo mzuri wa baada ya 2020. UNEP iliendelea kusaidia Sekretarieti ya CBD na Wanachama ili kuhakikisha mfumo huo unategemea sayansi na data ya hivi karibuni zaidi na kwamba uwajibikaji wa maendeleo ya kufikia ahadi zake za kimataifa unaimarishwa. Kwa kushirikiana na GEF na UNDP, UNEP pia imekuwa ikitayarisha mipango ya kusaidia mapema Wanachama kutekeleza mfumo pindi utakapopitishwa.

**UNEP-WCMC** ilishirikiana na UNDP na Sekretarieti ya CBD ili kutengeneza **Maabara ya Umoja wa Mataifa ya Bayoanuwai 2.0** - jukwaa lisilolipishwa la programu huria lililo na zaidi ya ramani 400 za hali ya juu na data kuhusu mazingira, mabadiliko ya tabianchi na maendeleo ya binadamu kama manufaa ya kidijitali kwa umma. Microsoft imejitolea kusaidia mfumo huo na **Kompyuta yake ya Sayari** na uchanganuzi maalum. Kufikia sasa, zaidi ya nchi 60 zimetumia data ya Maabara ya Bayoanuwai ya Umoja wa Mataifa kuandaa ripoti zao za kitaifa kwa CBD.



Kutokana na kupungua kwa kasi kwa idadi ya watu, Penguin wa Rockhopper "wamo hatarini". Picha: GRID-Arendal

Mwezi wa Mei mwaka wa 2021, Bodi ya Watendaji Wakuu wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa ya Uratibu iliidhinisha **Mtazamo wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa kwa Bayoanuwai**, kuunganisha suluhu za bayoanuwai na mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu katika sera na upangaji wa programu za Umoja wa Mataifa na utekelezaji. Kupitia mbinu ya pamoja, mfumo wa Umoja wa Mataifa umejitolea kujumuisha bayoanuwai na kuchochea hatua za pamoja kukabiliana na vyanzo vya uharibifu wa bayoanuwai, kuboresha mifumo ya ekolojia na hatimaye kuishi kwa amani na mazingira.

KUSHUGHULIKIA
**SAYARI**

# Kuboresha mifumo ya ekolojia duniani

**Tarehe 5 Juni, Siku ya Mazingira Duniani mwaka wa 2021, UNEP na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) zilizindua Muongo wa Umoja wa Mataifa wa Kuboresha Mifumo ya Ekolojia.**

FAO na UNEP kwa pamoja zimeanzisha Hazina ya Udhamini wa Washirika Wengi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli kuu za Muongo huu. Ahadi kuu kwa hazina hiyo zilijumuisha dola milioni 16 za Marekani kutoka kwa Ujerumani na dola milioni 11 za Marekani kutoka kwa Denmaki. Mwandalizi wa Siku ya Mazingira Duniani, Pakistan pia ilitoa ahadi thabiti kupitia mpango wake wa Kuchochea Upandaji Miti, ambao unalenga kulinda na kuongeza eneo lililo na misitu, kuunda maelfu ya ajira ya kupanda miti na kushughulikia mabadiliko ya tabianchi. **Zaidi ya nchi 100 zimetoa ahadi za kuboresha ardhi yao na ukanda wa pwani** kama sehemu ya ahadi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa bayoanuwai na uharibifu wa ardhi. Ahadi hizo zinafikia hadi zaidi ya hekta bilioni moja - eneo kubwa kuliko Uchina.

Iliyozinduliwa na UNEP na **Mpango wa Kimataifa wa Ardhi oevu** katika COP26, ripoti ya **Uchumi wa Uhifadhi wa Ardhi oevu, Uboreshaji na Usimamizi Endelevu wa Ardhi oevu** inabainisha sababu kuu ya usimamizi mbovu wa ardhi oevu kwa kutothamini manufaa yake ya kiuchumi. Inaangazia zaidi kwamba kutunza na kuboresha ardhi oevu kunaweza kupunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa kwa tani milioni 800 kwa mwaka - sawa na uzalishaji wa kila mwaka nchini Ujerumani. Ripoti hiyo ilitoa wito wa uwekezaji wa hadi dola bilioni 46 kila mwaka kufikia mwako wa 2050 ili kupunguza angalau nusu ya uzalishaji wa gesi chafu unaosababishwa na kuondoa maji na kuchoma ardhi oevu. Katika Global Peatlands Pavilion, iliyoongozwa na UNEP na washirika, Chile na Scotland zilitia sahihi makubaliano ya kuhifadhi ardhi oevu, huku Ireland ikijitolea kuanzisha Mradi wa Mboji Ulaya. Peru, Indonesia, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo pia ziliahidi kujumuisha maeneo ya ardhi oevu katika NDC zao.

## Usimamizi endelevu wa mazingira

UNEP na Wabia wa Mazingira na Upunguzaji wa Uwezekano wa Kutokea kwa Majanga walianza mwaka kwa Kozi mpya ya Massive Open Online ya **Masuluhisho kwa Majanga kutokana na Mazingira na Kustahimili Hali ya Hewa**. Zaidi ya watu 50,000 kutoka zaidi ya nchi 190 walijiandikisha kufanya kozi hiyo. Akiwa na umri wa miaka kumi, Indivara, mhitimu mchanga zaidi wa kozi hiyo, alisema, “Ilivutia sana, na ilinifanya nielewe njia za kina zaidi za jinsi unavyoweza kutumia mazingira kuokoa mazingira yenyewe.”

## Kubadilisha mifumo ya chakula ili kuwa na sayari endelevu na inayojumuisha zaidi

UNEP iliongoza Kikosi Kazi cha Umoja wa Mataifa kwenye **Mkutano wa Kilele wa Mifumo ya Chakula**, ambapo zaidi ya nchi 100 zilijitolea kufuata mikakati ya kitaifa kubadilisha mfumo wa chakula. UNEP na washirika pia wanaleta viongozi wa sekta hiyo pamoja kupitia **Mtandao wa Ufadhili wa Chakula Bora** ili kuhakikisha ufadhili wa mfumo endelevu wa chakula unakuwa jambo la kawaida.

Kabla ya Mkutano huo, Ripoti ya UNEP ya **Tathmini ya Uharibifu wa Chakula ya Mwaka wa 2021** ilionyesha kuwa watu huharibu karibu tani bilioni moja za chakula kila mwaka - karibu asilimia 17 ya chakula chote kinachopatikana kwa matumizi ya binadamu. Ripoti hiyo ilionyesha kwa mara ya kwanza kwamba uharibifu wa chakula hujitokeza katika karibu kila nchi, ikiwa ni pamoja na nchi za kipato cha kati na cha chini.

# Kushughulikia Mazingira




Bottle Reefs ni njia ya gharama nafuu ya kurejesha miamba ya matumbawe. Inaongeza sehemu ya kupandia matumbawe wakati wa kurejesha maeneo ya miamba ya matumbawe.
Picha: UNEP

## Kuzuia hatari za kiafya



Kukama nyoka aina ya Buka wa Australia.
Picha: Shutterstock

UNEP inafanya kazi na washirika wa Umoja wa Mataifa ili kuimarisha mbinu ya **One Health**, ambayo inatambua uhusiano kati ya watu, wanyama na mazingira. Hili litakuwa muhimu katika kukabiliana na majanga matatu ya sayari yetu. Katika mwaka wa 2021, G7 na G20 zote zilitoa matamko yanayounga mkono mbinu ya One Health.

UNEP ilisaidia **Kikundi cha Viongozi wa Duniani kuhusu Kushindwa Kukabiliana na Vijiumbe Maradhi** (AMR) na Jopo jipya la Ngazi ya Juu Linaloshauri One Health kuhusu uzuiaji wa janga. Juhudi hizi zitasaidia kuboresha sayansi kwa uingiliaji kati ulioratibiwa ili kuhakikisha usimamizi thabiti wa mazingira duniani ili kuzuia hatari za kiafya.

KUSHUGHULIKIA
**SAYARI**

## Kuhifadhi makazi na mifumo ya ikolojia

Mbuga ya Kitaifa ya Mlima Shar - iliyoanzishwa na Serikali ya Macedonia Kaskazini kwa msaada kutoka UNEP, GEF na wabia - iliandikisha historia mpya ya kutochafua mazingira nchini baada ya kampeni iliyochukua karibu miaka 30. Hifadhi hiyo mpya imechangia katika uundaji wa mojawapo ya maeneo makubwa zaidi yaliyohifadhiwa ambayo yamevuka mipaka barani Ulaya. Ikiwa na ukubwa wa hekta 67,000, ina spishi karibu 6,000 za wanyama na mimea mbalimbali, pamoja na Balkan Lynx aliye hatarini kutoweka, idadi yao ikisalia chini ya 35. UNEP pia ilisaidia Serikali ya Montenegro kuanzisha Maeneo mawili ya kwanza kabisa ya Bahari Yaliyohifadhiwa - hatua muhimu sana katika kufikia viwango vya kimataifa vya bayoanuwai.

Ripoti ya **Sita ya Hali ya Matumbawe Duniani inayoungwa mkono na UNEP: Ripoti ya Mwaka wa 2020** ilionyesha kuwa asilimia 14 ya matumbawe duniani yamepotea katika chini ya muongo mmoja kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Hii iliarifu mchakato wa **mfumo wa kimataifa wa bayoanuwai baada ya 2020**. UNEP, Hazina ya Umoja wa Mataifa ya Washirika Mbalimbali na wabia pia walichangisha zaidi ya dola za Marekani milioni 30 kupitia **Hazina ya Kimataifa ya Miamba ya Matumbawe** katika mwaka wa 2021. Hazina ya Kimataifa ya Miamba ya Matumbawe pia ilichangisha dola milioni 125 za ziada kupitia Hazina ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ili kusaidia uwekezaji wa kibinafsi kwa utunzaji wa miamba ya matumbawe.

Wakati huohuo, **Freshwater Ecosystem Explorer** program mpya – iliyoundwa na UNEP kwa ushirikiano na Kituo cha Utafiti cha Pamoja cha Tume ya Ulaya na **Google Earth Engine** – hutoa maelezo muhimu kuhusu jinsi mifumo mbalimbali ya ikolojia ya maji isiyo na chumvi hubadilika baada ya muda fulani katika kila nchi duniani kote.



Usafishaji wa ufuo Watamu, Kenya.
Picha: UNEP

## Kupunguza uchafuzi wa plastiki

Katika kipindi chote cha mwaka wa 2021, UNEP ilitetea juhudi za kimataifa za kushughulikia uchafuzi wa plastiki. **Kuanzia Uchafuzi hadi Masuluhisho: tathmini ya kimataifa ya uchafu wa baharini na uchafuzi wa plastiki** ya UNEP ilionyesha tishio linaloongezeka katika mifumo yote ya ikolojia. Ripoti hiyo inaangazia kwamba plastiki inachangia asilimia 85 ya takataka za baharini na inaonya kwamba kufikia mwaka wa 2040, kiasi cha uchafuzi wa plastiki katika maeneo ya baharini itaongezeka karibu mara tatu.

Kuna msukumo unaoongezeka miongoni mwa nchi kuhusu kuchukua hatua muhimu za kukabiliana na uchafuzi wa plastiki - huku Nchi Wanachama zikiongoza mijadala ya kikanda na kimataifa kuhusu takataka za plastiki baharini, ikijumuisha Jukwaa la Washika dau Mbalimbali kuhusu Takataka za Baharini na Plastiki Ndogo na Kongamano la Mawaziri kuhusu Takataka za Baharini na Uchafuzi wa Plastiki, yakiwa sehemu ya maandalizi ya majadiliano ya awamu ya pili ya **Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa** (UNEA 5.2).

# Kemikali na Kushughulikia Uchafuzi

## Kudhibiti uchafuzi wa hewa

Mwezi wa Septemba 2021, tathmini ya kimataifa ya **sheria za uchafuzi wa hewa**, ya kwanza kufanywa na UNEP, iliyochunguza sheria za kitaifa za ubora wa hewa katika Mataifa 194 na Umoja wa Ulaya, ilifichua kuwa nchi nyingi zilijumuisha viwango vya ubora wa hewa katika sheria, lakini ufuatiliaji wa utekelezaji unakosekana. Ripoti hio, iliyowasilishwa wakati wa maadhimisho **Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa Anga ya Bluu** ya pili, itatumika kama msingi wa kupunguza uchafuzi wa hewa kwa ufanisi zaidi.

UNEP imeungana na **IQAir** kuunda **mtandao wa uchafuzi wa hewa duniani**, mtandao mkubwa zaidi ulimwenguni wa kutoa data ya wakati halisi kuhusu ubora wa hewa duniani na maeneo yenye uchafuzi mkubwa zaidi. Katika majaribio ya kwanza ya aina hiyo barani Afrika, UNEP na kampuni ya mawasiliano nchini Kenya Safaricom walipeperusha moja kwa moja vipimo vya uchafuzi wa hewa kwenye mabango ya kidijitali mjini Nairobi.

Hili lilisababisha ongezeko kubwa la uhamasishaji wa ubora wa hewa na ushirikiano nchini Kenya na kusababisha ahadi kutoka kwa Safaricom ya kusambaza miundomsingi hiyo kote nchini Kenya na ikiwezekana kwa mataifa mengine.



Moshi unaotoka kwenye bomba la moshi kwenye mtambo wa kuzalisha umeme wa makaa ya mawe.
Picha: Shutterstock

Baraza hili ni taasisi ya ngazi ya juu zaidi ulimwenguni inayofanya maamuzi kuhusu mazingira, iliyo na Nchi Wanachama 193.

Mradi unaoongozwa na UNEP barani Asia ulibadilisha mienendo ya kuchakata tena huko Selangor, Malaysia, ambapo nia ya wakazi kushiriki katika utenganishaji wa taka imeongezeka hadi asilimia 75 majumbani katika baadhi ya maeneo ya jimbo hilo. Malaysia pia ilizindua sera mpya ya taka baharini katika hafla ya kila mwaka iliyoandaliwa kwa ushirikiano na UNEP.

Wakati huohuo, sayansi ya raia ilikuwa na wajibu mkubwa katika utafiti wa majaribio wa mradi wa **CounterMEASURE II** unaoongozwa na UNEP huko Asia, na kutafuta msingi wa uchafuzi wa mazingira kando ya mito, ambayo itatumika kupima mafanikio ya jitihada za kuupunguza.

Kote ulimwenguni, zaidi ya vijana 400,000 walishiriki katika kampeni ya **Wanaharakati wa Kupambana na Plastiki** mpango wa UNEP wa kubadilisha mienendo katika nchi 32, pamoja na kikosi cha vijana 2,000 waliofunzwa kushawishi sera kuhusu uchafuzi wa plastiki katika ngazi za mtaa, kikanda na kitaifa.

UNEP pia inashauri wafanyabiashara na serikali kutafakari kuhusu mustakabali wa plastiki **Ahadi Mpya ya Uchumi wa Plastiki Duniani**, inayoongozwa na UNEP na Wakfu wa Ellen MacArthur, ilileta pamoja zaidi ya kampuni kuu 500 zilizo na maono yaleyale la ya kutumia bidhaa tena na tena ili kusiwe na taka ya plastiki.

**Mkataba wa Basel** wa kudhibiti taka hatari zinazovuka mipaka pia ulifikia hatua muhimu katika mwaka wa 2021 wakati marekebisho yaliyopitishwa na nchi 187 ili kudhibiti kwa njia bora zaidi biashara ya kimataifa ya taka za plastiki, kuzuia uzalishaji wake na kuboresha usimamizi wake yalipoanza kutumika.

KUSHUGHULIKIA
SAYARI

## Kukabiliana na majanga ya mazingira



Uchafu uliosogea kwenye ufuo kutoka kwa meli ya kontena ya MV X-Press Pearl, Ja-Ela, Sri Lanka. Picha: Dinuka Liyanawatte/Reuters

Mwezi wa Juni mwaka wa 2021, Kitengo cha **Mazingira kwa ushirikiano wa UNEP-OCHA** kilishauri serikali kuhusu jinsi ya kudhibiti **mwanga wa sumu kutoka kwa X-Press Pearl** ufuoni mwa pwani ya Sri Lanka - ambapo mchanganyiko wa chembe za plastiki, kemikali na mafuta ulipelekea **tatizo la uchafuzi wa mazingira** changamano.

Mwezi huohuo, UNEP, Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Baharini (IMO), na washirika waliimarisha juhudi za kushughulikia majanga iwapo mafuta yatamwagika kutoka kwa **FSO Safer katika pwani ya Yemen**, ambapo karibu watu milioni 8.5 wanaweza kuathiriwa na viwango hatari vya uchafuzi wa mazingira ndani ya saa 36 za kwanza.

UNEP ilitumia teknolojia ya Kufuatilia Dunia ili kufuatilia matukio ya uchafuzi wa mazingira na kuimarisha shughuli za kuyasafisha nchini Israel, Lebanon, Sierra Leone na Syria.



Mchimbaji dhahabu akijaribu meza ya kutikisa isiyo na zebaki ili kufua dhahabu kwenye mgodi wa Aqua Azul katika wilaya ya Saramacca, Suriname.
Picha: Ranu Abhelakh/Reuters

# Kemikali na Kushughulikia Uchafuzi

## Kuondoa madini ya risasi yenye sumu kwenye mafuta na rangi



Mwaka wa 2021 uliashiria mwisho wa petroli yenye madini ya risasi baada ya **kampeni** ya karibu miaka 20 ya **Ushirikiano wa Kimataifa wa Mafuta na Magari Yasiyochafua Mazingira** iliyoongozwa na UNEP.

Kupiga marufuku matumizi ya petroli yenye madini ya risasi katika usafiri wa barabarani kumekadiriwa kuzuia zaidi ya vifo vya mapema milioni 1.2 kwa mwaka, kuongeza IQ za watoto, kuokoa dola trilioni 2.45 za Marekani kwa mwaka kwa uchumi duniani na **kupunguza viwango vya uhalifu**.

UNEP pia inasaidia nchi kukomesha madini ya risasi (Pb) kwenye rangi kupitia **Lead Paint Alliance**. Georgia, Morocco, Peru na Ukraine ndiyo mataifa ya hivi karibuni zaidi kupitisha sheria zinazozuia rangi yenye madini ya risasi, na hivyo kufanya jumla kuwa nchi 83.

Madini ya risasi katika maonyesho ya graffiti ya rangi.
Picha: UNEP

## Kupunguza madhara ya zebaki kwa afya na mazingira

Katika mwaka wa 2021, UNEP ilisaidia nchi 35 kukamilisha Tathmini ya Awali ya Minamata kwa kutumia Mercury Inventory Toolkit ya UNEP, na nchi 30 kuweka Mikakati ya Kitaifa ya uchimbaji dhahabu kwa kiwango kidogo, ambayo inaunga mkono utekelezaji wa **Makubaliano ya Minamata kuhusu Zebaki**. Dola milioni 44 za Marekani za ufadhili wa ziada ziliahidiwa kupitia mpango wa GEF **planetGOLD** unaoongozwa na UNEP na Conservation International, pamoja na ahadi kubwa ya ufadhili wa ushirikiano kutoka kwa wabia. Kampuni kuu tayari imejitolea kununua tani moja ya dhahabu isiyo na zebaki inayozalishwa chini ya mpango huo, yenye thamani ya zaidi ya dola milioni 50 za Marekani.



Kuonyesha jedwali jipya ambalo hutumia maji na mvuto pekee kama njia mbadala dhidi ya mbinu ya kawaida zaidi ya kutumia zebaki kufua dhahabu kutoka kwa madini.
Picha: Ranu Abhelakh/Reuters

KUSHUGHULIKIA
**SAYARI**

## Kuhamasisha kuhusu madini ya risasi hatari katika betri



Sekta ya uchukuzi ndiyo inayozalisha gesi nyingi ya ukaa, ikichangia takriban asilimia 25 ya uzalishaji unaohusiana na nishati.

Katika COP26, Mpango wa Kuharakisha Kuhamia Usafiri Unaotumia Umeme - sehemu ya **Mpango wa Usafiri Unaotumia Umeme** wa UNEP - ulizinduliwa ili kusaidia takriban nchi 30 za kipato cha chini na cha kati. Hii ni muhimu, kwani betri ya gari ya wastani ina karibu kilo 15 za madini ya risasi na ikiendelea kutumiwa inaweza kuchangia hadi kilo bilioni 20 za madini ya risasi kufikia mwaka wa 2050.

Betri zenye madini ya risasi zilizotumika zilizorundikwa ndani ya mtambo wa kushughulikia madini ya risasi. Picha: Robert Pratta/Reuters

# Kuifanya UNEP itimize kusudi



## Mkakati Mpya wa Muda Mfupi

Mwezi wa Februari mwaka wa 2021, Nchi Wanachama ziliidhinisha **Mkakati wa Muda Mfupi** (MTS) mpya wa UNEP wa 2022-2025 na **Programu ya Kazi** ya 2022-2023 ili kuimarisha uwezo wa UNEP wa kutekeleza kazi yake kama mamlaka inayosimamia mazingira duniani.

MTS inaeleza mchango wa UNEP katika **Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu** na **Muongo wa Utekelezaji**, na lengo la kuwa uendelevu wa sayari kwa watu, ustawi na usawa.

Mkakati huo unaenda sambamba na mifumo, utendakazi, utaratibu na utamaduni wa UNEP wa kuwa na athari kubwa zaidi inapofanya kazi yake.

UNEP pia inaweka kanuni za utenda kazi wake ili kushughulikia changamoto za muda mrefu na kuimarisha uwiano wa uwekezaji wa mradi na mfumo wa uwajibikaji.

## Kujitahidi kuboresha

Katika mwaka wa 2021, UNEP ilifanyiwa tathmini ya kina na **Mtandao wa Tathmini ya Utendaji wa Mashirika ya Kimataifa** (MOPAN), unaojumuisha nchi 21 ambazo zina nia moja katika kutathmini utendakazi wa mashirika makubwa ya kimataifa wanayofadhili.

Tathmini hii iliyoanzishwa na Ubelgiji, Uholanzi na Uswizi iliandaa maarifa huru, thabiti na ya kina kuhusu utendaji wa shirika la UNEP kuanzia katikati ya mwaka wa 2016 hadi mwaka wa 2020.

Ilionyesha kwamba UNEP *lilisalia kuwa muhimu sana na wajibu wake katika masuala ya kimataifa ya mazingira uliongezeka*. Utafiti kuhusu zaidi ya washirika 1,000 wa UNEP, makala 200 na mahojiano na zaidi ya wafanyakazi 40 vilitumiwa kama data ya tathmini ili kupata matokeo - na kupimwa dhidi ya mfumo wa kawaida unaotegemea utendaji bora wa kimataifa.

Tathmini hii pia iliangazia maeneo yanayohitaji kuboreshwa na UNEP, hasa ukusanyaji wa rasilimali na mchakato wa kubuni na kutathmini mradi.

## Uanuwai wa wafanyakazi


Kazi nyingi za UNEP katika mwaka 2021 zililenga kuendeleza uanuai wa wafanyakazi, kuanzia na uidhinishaji wa Ripoti ya UNEP ya Utekelezaji wa Usawa wa Kijinsia wa na Mpango wa Utekelezaji wa 2021-2023 - mwendelezo wa UNEP kwa **Mkakati wa Umoja wa Mataifa wa Usawa wa Kijinsia** wa Katibu Mkuu.

Wakati huohuo, UNEP ilipiga hatua thabiti kufikia na kupita malengo ya usawa wa kijinsia katika ngazi za chini na za juu zaidi za kitaaluma. Bado, kazi zaidi inahitaji kufanywa katika ngazi ya kati na juu, ambapo asilimia 43 ya wafanyakazi ni wanawake.


UNEP pia imejitolea kuongeza wafanyikazi kutoka kwa vikundi vya kikanda ambavyo vina uwakilishi mdogo ndani ya shirika. Kupitia hatua zilizolengwa za uhamasishaji katika mwaka wa 2021, UNEP ilifikia zaidi ya watu 600 wanaoweza kuajiriwa kutoka katika nchi mbalimbali, pamoja na watu 360 nchini Ukraine na watu 60 kutoka Urusi. UNEP pia iliboresha kuonekana kwake kama mwajiri anayependelewa kwa wale wanaopendelea kufanya kazi katika sayansi, mazingira, bayoanuwai, masuala ya mabadiliko ya tabianchi na maendeleo ya kimataifa.

# Ufadhili wa UNEP

## Bajeti, mapato na matumizi ya 2020 na 2021 (kwa pamoja)





## Wachangiaji 15 Wakuu wa Hazina ya Shughuli Maalum katika mwaka wa 2021
(mamilioni ya dola za Marekani)





**Ushirikiano kati ya UNEP na sekta ya fedha ulimwenguni ili kuhamasisha ufadhili wa sekta binafsi kwa maendeleo endelevu.

## **Wachangiaji 15 wakuu wa Hazina ya Mazingira katika mwaka 2021** (dola milioni za Marekani)




## **Wachangiaji katika Hazina ya Mazingira (2021) kulingana na kategoria ya** (idadi ya Nchi Wanachama)




Wachangiaji wa sehemu yao kamili* (39)

Wachangiaji kiasi kingine (41)

Wasiochangia (113)

*kulingana na kiwango kinachoonyesha michango



UN environment programme | 50 1972-2022

UN- Shirika la Mazingira
Barabara ya Umoja wa Mataifa
Gigiri, SLP 30552-00100
Nairobi, Kenya.

Chapisho hili linaweza kuchapishwa tena lote au kwa sehemu katika njia yoyote ili kuelimisha au kwa kusudi lisilo la kibiashara bila ruhusa maalum kutoka kwa wachapishaji halali mradi tu chanzo kitambulishwe. Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa litathamini kupokea nakala ya kitabu chochote ambacho kinatumia chapisho hili kama chanzo chake. Chapisho hili halipaswi kutengenezwa kwa kusudi la kuuzwa tena au makusudi mengine yoyote ya kibiashara kabla ya kupata ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa. Kujumuishwa kwa mashirika ya maeneo ya kijiografia katika ripoti hii, na uwasilishaji wa habari hapa, hakurejelei maelezo ya mawazo yoyote kwa upande wa mchapishaji au mashirika yaliyohusika kuhusiana na hali ya kisheria ya nchi, eneo au mahali popote, au ya mamlaka yake, au kuhusiana na kuweka mipaka yake. Sifa: Isipokuwa imeonyeshwa vinginevyo, data yote katika chapisho hili imetolewa kutoka kwa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa. Kwa habari zaidi: unep.org/ annualreport.
©Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa, 2022